

# TANGAZO!!!! TANGAZO!!!!!!

MKUU WA WILAYA YA MOMBA ANAWATANGAZIA VIJANA WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI ZA KUJIUNGA NA JESHI LA MAGEREZA WILAYA YA MOMBA KWA MWAKA 2023.

**MASHARTI NA SIFA ZINAZOTAKIWA;**

- (1) Awe raia wa Tanzania.
- (2) Awe amemaliza kidato cha nne na kupata ufaulu wa Daraja la I hadi IV.
- (3) Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 25.
- (4) Awe na siha njema.
- (5) Awe na amefuzu mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa (JKT) au aliyepo katika kambi ya JKT:
- (6) Asuwe amewahi kuajiriwa serikalini.
- (7) Asuwe ameo au kuolewa.
- (8) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili.
- (9) Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia mahakamani na kuhukumiwa kifungo.
- (10) Awe na urefu usiopungua futi 5'4 kwa wanawake na futi 5'7 kwa wanaume.
- (11) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya uaskari magereza.

**UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI NI KAMA IFUATAVYO:-**

Waombaji wote waandike barua kwa Mkuu wa Gereza wa Wilaya kwa anuani hii ("**Mkuu wa Gereza (W), S.L.P 205, MBOZI**") Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya posta.

**BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATANISHWE NA NAKALA ZIFUATAZO.**

- i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate).
- ii. Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne.
- iii. Nakala ya cheti cha kumaliza shule (Leaving Certificate).
- iv. Cheti cha utambulisho wa siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali.
- v. Nakala ya utambulisho cha uraia au namba ya utaifa kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- vi. Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la kujenga Taifa (JKT).
- vii. Picha nne (04) za passport size.


- viii. Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anakoishi mwombaji.

**NB:**

- i. Waombaji wote ambao walishafukuzwa katika kozi za mafunzo ya awali ya uaskari magereza hawaruhusiwi kuomba tena.
- ii. Barua itakayo wasilishwa kwa njia ya mkono au barua pepe (email) haitafanyiwa kazi.
- iii. Mwombaji yeyote atakaye wasilisha nyaraka za uongo/kugushi (Forged Documents) atakuwa ametenda kosa la jinai hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 05  
FEBRUARI, 2023.**

**IMETOLEWA NA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MOMBA  
LEO TAREHE 26/01/2023.**



Mary J. Marco

KATIBU TAWALA WILAYA

MOMBA